

MPENI MUNGU UTUKUFU

Na: Kidaha, D.R
05/05/2018, DAR

Kwa uchangamfu

6

1.A li u mba Mbi ngu na du ni a navyo te vi li vyo mo kwaku wa ye
A ka tu ka bi dhi wa na da mu i li tu vi ta wa le kwaku wa ye

ye a na u we za na u tu ku fu wote
ye ni mwenyengu vu na mwenye ku ta - wala mi le le m pe - ni m

11

Bwa na
pe ni Bwa na na he m pe ni u tu ku fu na u ku u m pe - ni m
m pe ni a he m pe ni a he m pe ni a he

15

Bwa Bwa na na
pe ni a he Bwa a na a he u tu ku fu na he shi ma m pe - ni m ma
a he a he a he a he a he a he a he

Bwa na

2. Tazama maji ya baharini yamewekwa mipaka,
Haijatokea siku moja yakavuka mipaka,
Kwa kuwa yeye aliyeumba kawekea mipaka,
Kwa kuwa yeye ni mwenye nguvu na mwenye kutawala milele, mpeni.....
3. Anatawala kama zote miaka pia miezi,
Na mwenendo wa sayari zote wafata amri zake,
Hakika ndiye mpanga yote na mwenye kutawala,
Hakuna wa kulingana naye duniani na huko Mbinguni, mpeni.....
4. Aliwatoa Waisraeli utumwani Mi-sri,
Akawavusha katika maji ya bahari ya Shamu,
Akawalisha mana jangwani walipopata njaa,
Akawapa maji kwenye mwamba kwa kupitia fimbo ya Musa, mpeni.....
5. Upendo wake ni wa ajabu tena unashangaza,
Alitupenda sisi wadhambi katupenda upeo,
Akamtoa mwanae pekee aje kutufia,
Kusudi sisi tuokolewe mwisho tufike kwake Mbinguni, mpeni.....
6. Hakika Mungu hafananishwi na kiumbe chochote,
Uweza wake na utukufu havina kadirio,
Akisema mvua isinyeshe hakuna wa kupinga,
Akisema mvua iwe nyangi yote hayo ni mapenzi yake, mpeni.....

NB: Isiende haraka sana. Mwendo wa maringo ndio raha yake.

Copyright: Kidaha the Hantinya
0765812333
deoraph@yahoo.com

Copied by Evodius Mwasanje
0758063937/0623488710/0719910915